AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Ajira

Kuwa na kazi itakusaidia kujenga mustakabali imara nchini Australia na wanaume pamoja na wanawake kwa jumla hutarajiwa kufanya kazi. Baada ya kuwasili nchini Australia, unaweza kukosa kupata kazi mara moja. Wewe unaweza kuhitaji kujifunza au kuboresha Kiingereza, pamoja na kusoma kabla ya wewe kupata kazi. Baadhi ya changamoto unazoweza kupatana nazo ni pamoja na:

- Hakuna uzoefu wa kazi katika Australia
- Kutokuwa na uwezo wa kuzungumza Kiingereza vizuri
- Kutokuwa na uwezo au kuwa na uwezo mdogo wa ustadi wa kutumia kompyuta
- Ukosefu wa mitandao ya kijamii ili kusaidia kutafuta kazi
- Kutojua wapi kutafuta kazi au jinsi ya kutuma maombi ya kazi
- Ujuzi ulionao unaweza kuwa hauhitajiki nchini Australia
- Sifa yako kitaalamu inaweza kukosa kutambuliwa katika Australia.

Huu unaweza kuwa wakati yanayokusumbua lakini ni sehemu ya mchakato wa kutulia ndani ya nyumba yako mpya. Kunazo huduma za bure ambazo zinaweza kukusaidia wewe kushinda changamoto hizi. **Kumbuka**: inachukua muda.

Wewe utahitajika kujifunza Kiingereza ili kupata kazi. Ni bora kukubali kazi unayoipata mara ya kwanza ili wewe uweze kuboresha ustadi wako katika sehemu ya kazi nchini Australia.

Idara ya Huduma za Binadamu (Department of Human Services) hutoa msaada wa kipato kwa watu wasiokuwa na ajira pamoja na huduma ili kuwasaidia watu kupata kazi au mafunzo. Serikali huwahimiza watu kutafuta kazi pamoja na kuendeleza ustadi wa kazi ili wasipate kutegemea msaada wa kipato. Ikiwa wewe unapata msaada wa kipato kwa kutokuwa na kazi unahitajika kutafuta kazi au unahudhuria elimu au mafunzo. Kwa habari zaidi, kwenda kwenye www.humanservices.gov.au

## Maadili ya kazi nchini Australia

Katika Australia, 'kufanya kazi' maana yake ni zaidi kuliko tu kutengeneza pesa. Kwa Waaustralia wengi, kuwa na kudumisha kazi ni sehemu muhimu ya utambulisho wao binafsi. Watu hawafikiri ni mbaya au makosa kuchukua kazi iliyo chini ya ustadi wako: inakupa uzoefu wa kufanya kazi nchini Australia na inaweza ikiwa inaongoza kwa kazi nyingine bora zaidi au mawasiliano na watu wanaoweza kukupa msaada pamoja na hutoa mapato kwa familia yako. Wanaume na wanawake wote hufanya kazi katika Australia na huchukuliwa kama wote ni sawa katika mahali pa kazi. Kuwa na 'maadili nzuri ya kazi' ni muhimu wakati una kazi. Hiyo ina maana unatendea kazi yako kwa umakini, hufanya vizuri na kujisikia radhi kwamba umefanya bora yako.



## Ushuru

Ushuru hukusanywa na Serikali ya Australia na hutumika kutoa huduma kwa jamii, kama vile shule, huduma za afya, barabara pamoja na ustawi. Ushuru hulipwa juu ya mapato ya chuma, kama vile mshahara kutoka kazi, mapato ya biashara, Ushuru wa Bidhaa na Huduma (Goods and Services Tax - GST) na riba ya akaunti ya benki. Kila mtu anayepokea mapato au msaada wa kifedha kutoka kwa Serikali lazima atie maombi ya kupata Nambari ya Faili ya Ushuru (Tax File Number - TFN) kutoka kwa Ofisi ya Ushuru ya Australia (Australian Taxation Office – ATO).
Kwa habari zaidi, nenda kwenye www.ato.gov.au

## Kupata kazi

Kupata kazi ni wajibu wako. Hii ni mojawapo ya hatua muhimu sana baada ya kuwasili katika Australia. Unaweza kupokea msaada wa jinsi ya kupata kazi, lakini utakuwa na jukumu kuu katika kutafuta, kupata na kutunza kazi. Ustadi za kompyuta ni muhimu katika kutafuta kazi na ajira.

Njia za kawaida kupata kazi ni:

- kuuliza marafiki na familia kama wanajua kazi yoyote (mitandao)
- kufuata ushauri wa Centrelink
- kujisajili na huduma ya jobactive au Huduma za Ajira ya Walemavu (Disability Employment Services). Kwa habari zaidi, kwenda kwenye:
    - www.jobs.gov.au/jobactive
    - www.dss.gov.au/our-responsibilities/disability-and-carers/programmes-services/disability-employment-services
- kwa kutumia tovuti bure ya JobSearch ya Serikali ya Australia. Kwa habari zaidi, kwenda kwenye www.jobsearch.gov.au
- kwa kutumia gazeti, bodi za kupasha habari kwa jamaa, tuvuti, pamoja na kitabu cha simu
- kutumia vyombo vya ajira ya kibiashara
- kuangalia magazeti ya biashara na mtaalamu
- kujitolea. Kufanya kazi kama kujitolea ina maana kufanya kazi bila kulipwa kwa mashirika ambayo huwasaidia watu wenye mahitaji. Inaweza kusaidia wewe kuendeleza ustadi pamoja na kupata uzoefu wa kazi. Watu wajitoleo wengine pia ni waamuzi bora ambao wanaweza kukusaidia kupata kazi ya mshahara. Kwa habari zaidi, kwenda kwenye www.volunteeringaustralia.org

Vinginevyo, wewe unaweza kutaka kuanzisha biashara yako mwenyewe. Serikali ya Australia hutoa habari na msaada. Kwa habari zaidi, kwenda kwenye www.business.gov.au

## Sifa kutoka nchi za ng'ambo

### Tafsiri ya sifa

Ni muhimu kuwa na sifa kutafsiriwa katika Kiingereza, na kujua kama sifa hizo zinatambuliwa katika Australia.
Wewe unaweza kupata kutafsiriwa vyeti vyako bure bila malipo yoyote kama ukiziwasilisha vyeti hizokwenye tuvuti ya www.translating.dss.gov.au

### Utambuzi wa sifa

Kuwa na sifa kutambuliwa rasmi kutaboresha nafasi yako ya kufanya kazi katika taaluma yako iliohitimu. Idara ya Elimu na Mafunzo hutoa habari juu ya jinsi ya sifa za kitaaluma cha nje ya nchi baada ya sekondari zitatambuliwa katika Australia. Baadhi ya biashara au fani hutoa kozi ya 'kuziba' ili kubadilisha sifa za nje ya nchi zifike viwango vya Australia.
Kwa habari zaidi, kwenda kwenye www.internationaleducation.gov.au

Kama una sifa katika viwanda vya uhandisi, ujenzi, kazi ya vyuma, umeme au upishi, Utambuzi wa Biashara ya Australia (Trades Recognition Australia - TRA) inaweza kutoa cheti cha biashara kutambuliwa Australia (hii si leseni).
Kwa habari zaidi, kwenda kwenye www.tradesrecognitionaustralia.gov.au/Pages/default.aspx



## Kupata Kazi

### Mahojiano

Kabla ya kupata kazi, unaweza kuulizwa na mwajiri kuhudhuria mahojiano ya kazi. Kunaweza kuwa watu wengi kushindana kwa kazi hiyohiyo. Wakati wa mahojiano utahitaji kueleza uzoefu wa kazi yako na elimu. Katika baadhi ya tamaduni, si heshima kwa watu kuzungumza juu yao wenyewe. Hata hivyo, katika Australia, unahitaji kuelezea uzoefu wako, ujuzi, na sifa kwa mwajiri wako kwa kuongeza nafasi yako ya kupata kazi. Vinginevyo, mwajiri hajui kuhusu ujuzi na uzoefu unao kutoa. Wewe umeshaonyeshwa ujasiri na uamuzi mengi juu ya safari yako kuja Australia. Hizi ni sifa nzuri ambazo mwajiri atapenda.

### Wasifu

Wasifu mara nyingi huombwa wakati unapo omba kazi. Zinawajulisha mwajiri wa uzoefu wako wa kazi uliopita, sifa zako, na asili. Wasifu ichapishwe kwenye kompyuta na kuangaliwa kwa makini kwa makosa ya herufi. Unaweza haja ya kurekebisha wasifu yako kwa kazi maalumu. Ikiwa wewe hauna uzoefu wa kazi unapaswa kusema kazi ngani ya hiari, au kozi za mafunzo, ambazo wewe umeshafanya au jinsi uzoefu wa maisha yako hukuandaa wewe kwa ajili ya kupata kazi. Huduma kama vile jobactive inaweza kukusaidia wewe kuandaa wasifu yako. Kwa habari Zaidi, kwenda kwenye www.jobs.gov.au/jobactive

## Punde tu unapopata kazi

Kuwa na **maadili ya kazi** yeney nguvu itakusaidia kutunza kazi yako. Hapa ni baadhi ya vidokezo:

- Fika kwa wakati; usichelewa kamwe. Kama una tatizo na hawezi kufika kwa wakati, hakikisha unapiga simu na kumshauri msimamizi wako haraka iwezekanavyo
- Kuwa uzalishaji mali; jishughuliki katika masaa ya kazi.Chukua mapumziko wakati mapumziko yamepangwa
- Matatizo madogo ya binafsi ni udhuru kwa kukosa kwenda kazini. Acha kwenda kazi tu kama wewe ni dhati ya wagonjwa au una dharura
- Uliza maswali kama wewe huelewi kazi. Uliza mfanyakazi mwingine au bosi wako
- Uwe mwangalifu, kujifunza kwa kuangalia wengine
- Usikuwa mtazamaji tu. Chukua hatua na kujifunza kazi mpya au uliza kama unaweza kuchukua majukumu mapya
- Jenga uhusiano mzuri na wafanyakazi wengine, lakini kuwa mwangalifu kwa kuacha kutumia muda sana kuongea kijamii wakati wa masaa ya kazi
- Watendee wengine kwa heshima. Utakuwa unafanya kazi na watu kutoka tamaduni nyingine, dini na maoni. Kumbuka kwamba katika mahali pa kazi, wanaume na wanawake wanatendewa kwa usawa
- Kujenga rekodi imara ya kazi, kaa katika kazi hiyo kwa angalau miezi sita kama inawezekana
- Kila mara mpe mwajiri wako ilani iwezekanavyo kabla ya kuacha kazi. Watakuwa waamuzi wako kwa kazi yako ijayo kwa hiyo ni lazima kuwatendea kwa heshima na adabu
- Kulingana na sheria lazima uwaeleze Centrelink ili aweze kurekebisha malipo ya usaidizi wa mapato.






Ukurasa huu umewachwa tupu makusudi

*Toleo la Marekebisho (Aprili 2018)*

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM